# LEARNING BY EAR

## ”WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA DHIDI YA MALARIA”

## KIPINDI CHA SITA:MCHEZO WA LAWAMA, LAWAMA SI SULUHISHO.

**SCRIPT: CHRISPIN MWAKIDEU**

**EDITOR: ANDREA SCHMIDT**

**ASSISTANT EDITOR: Katrin Ogunsade**

**HEALTH EXPERT: DR. HEIDRUN HÜBNER**

**List of characters for episode 6:**

- MASIKA (40)
- BETTINA (34)
- KAREMBO (14)
- ZAWADI (BABY, no actor)
- MAMA DAVID (43)
- DR.MUNGA (45)
- DUTY NURSE (24)

**INTRO/NARRATOR (same voice):**

Sina shaka hujambo msikilizaji na kwa moyo mkunjufu nakualika tena katika kipindi cha Noa Bongo Jenga maisha yako tukiendelea na mchezo wa kuigiza kwa jina **WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA – VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA".** Katika sehemu ya tano wiki iliyopita Betina alimuongopea mume wake na kuwapeleka karembo na zawadi kwa mganga ili wapate matibabu... karembo alipobashiri haya naye kwa hofu licha ya kudhoofishwa na ugonjwa alimdanganya mamake na kutoroka kwa mganga...Na Masika nae anajuta anapofahamu kuwa amekuwa kielelezo kiovu kwa wavuvi wenzake wakiongozwa na Yakubu alipomwambia kuwa wanatumia neti za kujikingia mbu kinyume na matumizi yake,kuvulia samaki..katika hospitali ya mji wagonjwa furi furi wanamiminika kutokana na maambukizi ya malaria... je karembo anatorokea wapi? Je, Mganga Mizanja atafaulu kumtibu zawadi? Ni nani wakulaumiwa? Kwa haya na zaidi tusikilize kisa **"MCHEZO WA LAWAMA , LAWAMA SI SULUHISHO!"**tujiunge naye Daktari Munga akijaribu kuokoa maisha ya mgonjwa mmoja.

**MUSIC INTERLUDE**

**<u>SCENE ONE: EMERGENCY AT RIBO DISTRICT HOSPITAL</u>**

**A-SFX: SOUND OF BED BEING WHEELED ON FLOOR**

**DR. MUNGA: (HURRIEDLY)**

Samahani..fanyeni haraka ..tafadhali,anapoteza fahamu!

1. **DUTY NURSE:** Daktari,pumzi zake zinaonekana kukatika.

2. **DR. MUNGA:** Mtazame mdundo wake wa moyo!

**3. DUTY NURSE:** Uko kwa mbali sana..ni dhaifu nina hofu tutampoteza

**4. DR. MUNGA:** Mtie upepo wa msaada hivi sasa...

**5. DUTY NURSE:** **(BREATHING INTO PATIENT)**
Moja! Mbili! Tatu!!(**BREATHES IN AGAIN)**
tumechelewa Daktari.. tumempoteza.. (**SADLY)**

**6. DR. MUNGA:** (**FEELING BEATEN)**
La, hatukuchelewa bali yeye ndiye aliyechelewa kuja hospitali.

**NARRATOR:** Na uhai mchanga ukatoweka kwa ajili ya malaria, kutotafuta matibabu mapema ni chanzo kikubwa cha kutoweza kuidhibiti malaria hata kwa madaktari wenye ujuzi kama Munga..kwengineko, nyumbani kwa Masika, Betina alirudi bila tiba yeyote baada ya kuelezwa na Mizanja kuwa ni sharti awaaguwe wakiwa wote familia nzima Masika, betina, karembo na zawadi kwani pepo mchafu haaguliwi nusu nusu.

**<u>SCENE TWO: MASIKA'S HOME</u>**

**7. B-SFX: DOOR BEING OPENED AND BANGING**

**8. BETTINA:** **(ANGRY)**
Karembo! Karembo! Kwanini Karembo kunifanyia hivi? Kwanini?

**9. C-SFX: BABY STARTS TO CRY**

**10.** **BETTINA:** Hebu nyamaza zawadi!
(**BETTINA STARTS TO CRY TOO)**

**11.** **MASIKA:** (**CONCERNED)**
Mke wangu, kuna nini? Hebu mlete huyo mtoto...

**12.** **D-SFX: BABY STOPS CRYING MAKES SOME BABYISH NOISES**

**13.** **BETTINA:** Karembo yuko wapi?

**14.** **MASIKA:** **(PUZZLED BY QUESTION)**
Kwani hukwenda naye sokoni? Hapa nyumbani hayuko basi!

**15.** **BETTINA:** **(REGISTERING SHOCK)**
Ati?**,** Karembo hayuko huku?,una hakika?

**16.** **MASIKA:** Kuna nini? Yuko wapi binti yangu?,kumetokea nini?

**17.** **BETTINA:** Wuui! Twende masika... twende!!!

**18.** **MASIKA:** Twende wapi? nataka kujua binti yangu yuko wapi? Uliondoka naye na sasa hukurudi naye... mimi sitanyanyuwa mguu wangu hata hatua moja sharti unileze binti yangu Karembo yuko wapi?

**19.** **BETTINA:** Sawa.. nitakueleza... lakini niahidi utanisamehe... tafadhali...

(**BREAKS DOWN IN TEARS)**

**NARRATOR:** Na betina alipoanza kumsimulia mumewe yale aliyoyafanya, Karembo alikuwa ameshafaulu kufika milango ya hospitali ya wilaya ya Ribo.

**(AT RIBO HOSPITAL)**

**20. E-FX: WIDE DOORS SWINGS OPEN IN AND OUT**

**21. KAREMBO:** Nisaidiee..(**FAINTLY)** tafadhali nisaidie.

**22. DUTY NURSE:** **(HURRYING TO HELP)** Mungu wangu! Jikakamue msichana... usijali sasa uko mikononi mwetu.

**NARRATOR:** Aliposikia maneno hayo ya kutia moyo, karembo alipoteza fahamu.. aliona wingu jeusi, kimya kikatanda na ghafla akazimia mikononi mwa muuguzi aliyemchukua na kuanza kumuhudumia... kule nyumbani nako, betina na masika waliamua kumsaka karembo kila mahali. Waliingia kila kijumba cha jirani kumuulizia na wa kwanza alikuwa mamake david.

<u>**SCENE THREE: AT MAMA DAVID'S HOUSE**</u>

**23. MASIKA:** (**ANGRILY)** Yani uliniongopea na ilihali ulijuwa vyema karembo ni mgonjwa? Siamini! kisha ukamdanganya na yeye pia, alipogunduwa ndio akatoroka bila kukujulisha alikoenda...

**24. BETTINA:** Hebu usinilaumu mimi tu,ala!wewe pia ulichukua neti ya mbu bila hata ya kujali nitahisi vipi sababu yako zawadi pia ameambukizwa.

**25. MASIKA:** Ala! Kwahivyo lawama ni kwangu sasa? Mimi ndiye wakulaumiwa kwa kila kitu sio? Hapana! Sikubali! Ungelinieleza ukweli lakini kwa ajili ya uwerevu wako wa kijinga... sasa tumempoteza msichana wetu ambaye ni mgonjwa... hatujui aliko...na hata kama amekumbwa na...

**26. BETTINA:** Hebu nyamaza fikra zako mbaya... masika binti yangu ni mzima... najuwa ni mzima...

**27. MAMA DAVID:** **(INTERRUPTING BY COUGHING)** Samahani... hapa kuna shida kubwa na nyinyi ni kugombana na kulaumiana.. hilo halisaidii. karembo ametoweka, ni lazima tumtafute... na tumpate! Najua ni vigumu lakini kuna mahali patatu ambapo tunaweza kuanzia..polisi,hospitali na

hmm..

**28. BETTINA:** **(STARTS TO CRY)**

La! Karembo ni mzima!!! Yuko hai..

**(TURNS TO MAMA DAVID)**

Yote ni wewe!! Ndio! Wewe mama david.. ningelikuwa na mwanangu sasa laiti sio wewe kunishurutisha nimpeleke karembo kwa mizanja (**SOBBING)**

**29. MASIKA:** **(WITH RAGING ANGER)**
Kumbe hata wewe mama david pia unahusika? Iwapo chochote kitampata binti yangu mujuwe nyote wawili muko lawamani... na usithubutu tena kuikaribia familia yangu!! Nyoka wewe! Tuache na hamsini zetu na wewe chukuwa hamsini zako!! Twende mamake kiza kinazidi... na la mwisho... usinunuwe tena samaki kutoka kwangu!!!

**NARRATOR:** Hamaki ilimjaa masika akawa anawaka kama moto wa kuotea mbali... aliipa kisogo nyumba ya mamake david. Guu mosi Guu pili akiwa amembeba zawadi wote wakaelekea hospitali ya Ribo kumtafuta karembo. Kule hospitali nako taratibu... karembo alikuwa akipata afueni....

**MUSIC INTERLUDE**

**SCENE FOUR: MALARIA WARD AT RIBO DISTRICT HOSPITAL**

**30. DR. MUNGA:** **(WARMLY)**
Hujambo msichana?, jina langu ni Daktari Munga... wewe unabahati sana... ulikuja na ulipofika tu ukazimia.. tulipata wakati mgumu sana kukurudisha katika fahamu zako,hatukutaka kupoteza maisha zaidi.

**31. KAREMBO:** (**FAINT VOICE)**
kwani niko wapi? Babangu na mamangu wako wapi? Hmmm..

**32. DR. MUNGA:** **(REASSURINGLY)**
uko katika hospitali ya Ribo.. usijali tutawatafuta

wazazi wako.. tulikufanyia utafiti tukakukuta una malaria nyingi sana ndio sababu tulianza matibabu mara moja ya kuinini ya maji ili upate nafuu ya kuanza kumeza dawa mwenyewe... kwa sasa utaendelea kupumzika tu…...

**33. KAREMBO:** Hapana! Nahitaji kuwaona wazazi wangu... hawajui niliko.

**34. DR. MUNGA:** Kwani unaitwa nani na unaishi wapi?

**35. KAREMBO:** Karembo..Karembo Masika. Naishi karibu na mto na babangu ni mvuvi...

**36. DR. MUNGA:** Hilo ni eneo lililo na mkurupuko wa malaria! Nilisikia kupitia redio kuwa wavuvi wa eneo hilo wamegeuza neti za kukingia mbu zilizotibiwa na dawa ya kuua wadudu kuwa nyavu za kuvulia samaki... hayo ni mauti! Kwa sababu bado watu wanamiminika kutoka eneo hilo wakiwa na malaria... haswa kina mama waja wazito na watoto chini ya umri wa miaka miaka mitano.

**37. F-SFX: WIDE DOOR SWINGS OPEN, IN AND OUT**

**(MASIKA AND BETTINA FINALLY FIND KAREMBO)**

**38. BETTINA:** **(OVERWHELMED WITH JOY AND TEARS)** Mwanangu!! Nashukuru Mungu wangu...

**39. DR. MUNGA:** Bila shaka nyinyi ni wazazi wa huyu binti... basi tulieni na muzuie hisia zenu... msichana wenu yuko salama na ana ujasiri sana

**40. MASIKA:** Ndio... sisi ndio wazazi wake... tunafurahi sana kukuona tena karembo... tulihofia madhara yangelikupata.. bwana daktari.. tunafursa ya kurudi naye nyumbani?

**41. DR. MUNGA:** Kwa sasa la.. lazima tuwe naye karibu ili tumuangalie hali yake kwa kipindi cha masaa 48, kwa sasa ninapendekeza mumuache abakie hapa... pia ningelitaka kujua chochote kinachohusu afya yake.,kwa mfano ni lini alianza kuonyesha ishara au dalili za malaria... kama muliwahi kumpa dawa zozote nyumbani munieleze ,na maelezo mengine yeyote muhimu...

**42. MASIKA:** Labda atakueleza mwenyewe... lakini ninachofahamu ni kuwa nilimpa dawa za kutibu malaria na hazikumsaidia kamwe... sijui kama zilikuwa zimeharibika au vipi?

**43. DR. MUNGA:** Sidhani... nashuku ulimpa dawa ambazo hazitumiki tena kutibia malaria... malaria inatatiza kwa sababu inazidi athari ya dawa zinazotumiwa kila wakati...dawa kama klorokuini ni rahisi na salama lakini vimelea vya malaria havidhuriki na dawa hizo...

**44. MASIKA:** Sina habari... mke wangu, kwa vile tumempata Karembo , na tuko hospitali.. kwanini tusimpeleke zawadi naye akaangaliwa?

**45. BETTINA:** Hapana! Sio zawadi pekee... lakini sote tungelipimwa ikiwa tuna malaria... ndio turudi nyumbani...

**46. DR. MUNGA:** Hilo ni wazo zuri... tafadhali nendeni mkajiandikishe kwa matibabu... alafu mutakwenda katika maabara mwisho wa huo ukumbi mkono wako wa shoto .. nahitaji kuwaona wagonjwa wengine.. shukrani kuwajuwa...

**47. MASIKA:** Asante daktari.

**48. DR. MUNGA:** Tutaonana baadaye.

**OUTRO/NARRATOR:** Na hivyo basi familia ya masika ilikusanyika pale alipokuwa binti yao anauguza malaria, walifurahi kumpata na kumuona salama... hata kama alionekana mgonjwa na chupa za maji zikinin’ginia juu yake wote walijuwa yuko katika mikono salama... walipomaliza kujiliwaza na kufutana machozi ya furaha, betina,masika na mtoto wao zawadi walikwenda kupimwa. je matokeo yatakuwa yapi? Je, karembo atalazwa hospitali kwa muda gani na je huku hakutazua utata katika kufuzu kwake kwani mtihani wa kitaifa ulikuwa unabisha hodi ...je, ujirani wao na mamake david utarudi ulivyokuwa ama ndio umekatika baada ya kuwapa ushauri wa kwenda kwa mganga Mizanja? Basi kwa haya na mengineyo... Usikose sehemu ya saba ya mchezo ” **WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA**

**MOJA DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA”** kumbuka kwa kusikiliza tena au kutuma maoni yako tembelea tovuti zetu www.dw-world.de/lbe